MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA

**Na: 6. Msimu wa kilimo 2017/18 Tathmini ya Kipindi cha Novemba 11-20, 2017 na matazamio kwa kipindi cha Disemba 1-10, 2017**

**MUHTASARI**


- Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua, wakulima wanaendelea na shughuli za palizi isipokuwa baadhi ya maeneo ya Mkoa wa shinyanga ambao bado wanapanda.
- Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa Mvua, mvua za msimu zimeanza kwa maeneo ya Kigoma, Rukwa na Tabora ambako wakulima wameanza kupanda
- Kutokana na hali ya ukavu wa muda mrefu kwa maeneo mengi ya Shinyanga, Dodoma, Singida, Longido ns Kiteto, wafugaji wanashauriwa kutumia malisho na maji kwa uangalifu.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-31, 2017

Katika kipindi tajwa, migandamizo ya hewa iliyo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu wakati migandamizo iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kuimarika, hivyo kuruhusu ukanda wa mvua (ITCZ) kuelekea kusini mwa dunia. Joto la Bahari katika Bahari ya Hindi iliendela kuwa juu kidogo ya Wastani ambalo lilisababisha maeneo ya Pwani kuwa na vipindi vya mvua. Kwa upande mwingine joto la bahari la juu ya wastani liliendelea kuongezeka katika eneo la Kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) hali iliyosababisha kupungua kwa mvua katika maeneo ya Magharibi mwa nchi na Ukanda wa Ziwa Viktoria.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-31, 2017

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa, mvua zinazozidi wastani kwa zaidi ya milimita 50 zilinyesha katika maeneo ya Kagera, Tabora, Ruvuma, Shinyanga, Singida and Songwe kama inavyoonekana kwenye kielelezo. Vilevile mvua za zaidi ya mm 100 zilinyesha katika maeneo machache ya mkoa wa Ruvuma, Tanga, Tabora, Shinyanga, Mara and Kagera. Maeneo machache ya mkoa wa Rukwa, Morogoro, Kilimajaro na Tanga yalipata mvua za chini ya wastani kati mm 20 hadi 50 kama inavyoonekana kwenye kielelezo.




**Kielelezo**. Mwenendo wa mvua katika kipindi cha Tarehe 21-31 Novemba , 2017.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-31, 2017

Mvua zilizonyesha katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua zimesaidia kuimarisha unyevunyevu kwenye udongo kwa shughuli mbalimbali za kilimo. Wakulima wameendelea na palizi hususan maeneo ya kanda ya ziwa Viktoria, pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki isipokuwa mkoa wa Shinyanga ambapo wakulima wameanza kupanda. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kama mkoa wa Tabora, Rukwa na Kigoma msimu wa mvua umeanza na wakulima wanapanda mazao. Maeneo yaliyosalia wakulima wanaendelea na

maandalizi ya mashamba kwa ajili ya msimu unaotarajiwa kuanza wiki ya nne ya Novemba hadi Disemba. Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo ulikuwa wa wastani katika maeneo mengi ya nchi kutokana na mvua za *Vuli* zinazoendelea kunyesha, isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya Simiyu, Shinyanga, Dodoma, Singida, Longido na Kiteto ambako hali ya maji na malisho bado si ya kuridhisha.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-31, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito vimeanza kuongozeka hususan maeneo yanayopata misimu miwili wa mvua kutokana na mvua za vuli zinazoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2017

Migandamizo iliyopo Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) itaendelea kuimarika. Vilevile mgandamizo uliopo kusini (St. Helena) nao pia utaanza kuimarika, wakati mgandamizo mwingine wa kusini (Mascarene) utaendelea kudhoofika hivyo kusababisha Ukanda wa mvua (ITCZ) kuendelea kubaki Tanzania hususani katika meneo ya nyanda juu kusini magharibi na mikoa ya kusini. Mifumo hii itapelekea ongezeko la mvua katika maeneo hayo. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la Kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi na hivyo kusababisha mvua katika maeneo ya ukanda wote wa pwani. Kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki kunatarajiwa kuendelea kuwepo kwa joto la juu ya wastani na hivyo kupunguza mvua katika Magharibi mwa nchi na Ukanda wa Ziwa Viktoria.

## HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2017

Maeneo ya **kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara, Geita, Simiyu na Shinyanga)** na maeneo **ya Kati (Mikoa ya Dodoma na Singida)** yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua vitakavyoambatana na ngurumo katika maeneo machache**. Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara), Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Tanga, visiwa vya Unguja na Pemba)** na **Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi)** yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Iringa, Njombe, Songwe na Mbeya), Kusini (Mkoa wa Ruvuma)** na **Magharibi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora)** yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

## MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2017

Mvua zinazotarajiwa zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa ajili ya mazao na malisho. Wakulima wanashauriwa kuzitumia mvua hizi kwa shughuli za kilimo kama kupanda na kupalilia. Ambako mvua za msimu hajijaanza wakulima wanashauriwa kuendelea kuandaa mashamba.Vilevile wakulima na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani na kuchukua hatua stahiki.Wafugaji wanashauriwa kutumia malisho na maji kwa uangalifu

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa mito kinatarajiwa kuongezeko kidogo katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka hususan bonde la maji la Ziwa Viktoria, Rufiji, Pangani na Wami/Ruvu. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuendelea kuyatumia kwa uangalifu.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

*S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 Baruapepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet1_tz@meteo.go.tz*